



# KUDHIBITI



**UGONJWA WA MDONDO**



## **KUDHIBITI UGONJWA WA MDONDO**



### **NA NJIA ZA KUZUIA**

- 1 Soma maelezo yanayoambatana na kila kielelezo na kisha ufanye mazoezi ya kutoa mada ukiwa nyumbani kabla ya kutoa mada kwenye mhadhara.
- 2 Onyesha kila kielelezo kwa namna ambavyo watu wote watakiona vizuri, na waulize ni kitu gani wanakiona katika kielelezo hicho.
- 2 Baada ya makubaliano ya kuwa kielelezo hicho kinaonyesha nini, basi waweza kutowa maelezo yanayoambatana na kila kielelezo





## **Kumbuka:Mada kwa mdomo inaanza hapa!**

### **Kielelezo 1.Umuhimu wa Kuku wa asili**

Kuku ni kitoweo muhimu na pia chanzo cha mapato kwa familia nyingi hapa Tanzania.

Familia nyingi hufuga kuku kuliko aina nyingine ya wanyama

Kuku hukua haraka pia ni rahisi kuwafuga kila mmoja kwenye familia anaweza kufuga kuku.


Kuku hutupatia nyama na mayai ambavyo vyote ni muhimu kutufanya tuwe wenye nguvu na afya.

Kuku na mayai pia vinaweza kuuzwa kwa urahisi ili kutupatia fedha kila tunapoziitaji.Tunapohitaji kiasi kidogo cha fedha kama vile kwa ajili ya kununua dawa,daftari,na vitabu vya shule ni vema kuuza kuku au mayai kuliko kuuza ng'ombe au mbuzi.

Kuku ni muhimu wakati wa sherehe na sikukuu mbalimbali,vile vile kuku ni rahisi kuandaliwa kwa ajili ya chakula wakati wa ugeni wa dharura.


Kwa hiyo inatupasa kuwafuga kuku wetu vizuri.

Leo tutazungumzia namna ya kuwalinda kuku wetu dhidi ya ugonjwa unaoua kuku wetu vijijini kila mwaka.



## **Kielelezo 2.**

### **Tabia za ugonjwa wa mdondo**



Ugonjwa wa mdondo ni tatizo kubwa kwa wafugaji wa kuku kote duniani.

Katika Tanzania, ugonjwa wa mdondo unasababisha vifo vingi kwa kuku wanaofugwa vijijini na katika maeneo ya viunga vyamiji.

Mbali na ugonjwa wa mdondo, kuna magonjwa mengine yanayo sababisha vifo vyakuku

Magonjwa gani hayo?


Mdondo ni ugonjwa unaoua kuku wengi kuliko ugonjwa mwingine wowote wa kuku.

kwa hiyo tunatakiwa tuweze kutambua tabia za ugonjwa huu.

Ugonjwa wa mdondo umepewa majina mengi kutegemeana na nchi na nchi na wakati mwingine kati ya wilaya na wilaya.

Kwa mfano nchini Tanzania ugonjwa huu unaitwa Mdondo.

Hapa kwenu ugonjwa wa mdondo mnauitaje?





### **Kielelezo 3.**

### **Kushusha mabawa**


Angalia picha hii. Unaweza kuona nini?

Mabawa ya kuku yameshuka. Baadhi ya nchi, wafugaji husema kuku amevaa koti au koti linajiburuza chini.

Manyoya yake yamesimama.

Wakati mwingine kichwa huvimba.






#### **Kielezo 4.**


#### **Mharo wa rangi ya kijani**

Tafadhali elezea unaona nini katika picha hii.

Kuku ameharisha mharo wa rangi ya kijani. Hii inamaanisha kwamba kuku wanapotoa kinyesi hutoa majimaji ya kijani badala ya kinyesi kigumu.

Mharo huo kuchafua manyoya ya kuku sehemu ya nyuma ya kutolea haja.









## Kielezo 5.


### Shingo iliyopinda

Picha hii inaonyesha nini?

Picha hii inaonyesha shingo ya kuku imepinda na manyoya yamesimama.

Mara nyingi atapata shida katika kupumua.





Kielelezo 6.  
Vifo vingi

Kitu gani kinatokea hapa?

Kuna Kuku wengi wamekufa.  
Ugojwa gani unaweza kusababisha vifo vingi vya kuku?

Mudondo husababisha vifo vingi kwa muda mfupi.





## **Kielezo 7. Hakuna matibabu**

Tunaweza kuona nini?

Tunaweza kumuona mwanamke na mwanaume.


Mwanamke ana kuku mgonjwa.


Mwanaume amebeba sinia lenye vitunguu saumu, sabuni ya unga na pilipili.

Umeshawahi kutumia matibabu kama haya Kutibu au kukinga kuku wako? Yalifanya kazi?

Je unajua tiba nyingine ya asili?

Wakati gani unatumia tiba hiyo? Wakati tayari kuku wameshaugua au kabla hawajaugua?





### **Kielelezo 8.**

#### **Ndege wengine wanasambaza ugonjwa huu**

Ndege gani tulionao hapa ?

Tunaye Bata Mzinga, njiwa, bata na kanga.

Ndege hawa wanaweza kueneza ugonjwa wa mdondo.

Bata mzinga na Njiwa wanaweza kuugua ugonjwa wa Mdondo.

Kanga hawawezi kuugua mdondo lakini anaweza kubeba virusi vinavyosababisha ugonjwa huo na kuwaambukiza kuku.

Bata wakubwa wanaweza kupata ugonjwa wa mdondo lakini hawafi . Hata hivyo, vifaranga vyataga vinaweza kuugua mdondo na kufa.

Ukiona bata wa umri wote wanakufa kwa ugonjwa, ni kwa sababu ya ugonjwa mwingine unaoshambulia bata na siyo mdondo.



Kilelezo 9.

Jinsi ugonjwa unavyoenea

Hapa tuna mchoro wenyewe sehemu nyingi.

Mchoro unaonyesha baadhi ya njia ambazo

ugonjwa wa mdondo unaweza kuenezwa.

Tutaangalia sehemu moja baada ya nyingine.

Katikati kuna kuku mwenye afya nzuri.

Kuku huyu amezungukwa na miduara yenyeye picha  
mbali mbali ndani yake.

Mduara wa juu tuna kuku ambaye ameharisha (kinyesi cha  
majimaji). Kulia kuna mbwa anaye kula mzoga wa kuku, halafu  
yanafuata mayai, baada ya hapo linafuata gari. Duara linalofuata  
kuna mabaki ya kuku aliyechinjwa manyoya, mifupa na viungo vya  
ndani. Mduara wa mwisho una mwonyesha binadamu na nyayo  
zake.

Mdondo unasababishwa na vijidudu vidogo vidogo sana  
(virusi) ambavyo hatuwezi kuviona kwa macho yetu. Kwa  
mfano mdudu kutoka kwenye kuku mgongwa anaweza kukaa  
katika ganda la yai na kusafirishwa hadi katika maeneo  
mengine yasiyo na ugonjwa. Pia vijidudu vinaweza  
kusafirishwa katika viatu, matenga ya kusafirishia kuku,  
vikapu pamoja na magari.

Una maswali kuhusiana na mchoro huu ?








### **Kielelezo 10.**

### **Namna ninavyoweza kuwa na kuku mwenye afya**


Picha hii inatuonyesha nini ?

Tunamwona mwanamke ambaye ana wasiwasi juu ya kuku wake. Anawaza ni kwa jinsi gani anaweza kufuga kuku wenyе afya.



Kielelezo 11. Kuchanja kuku  
Unaweza kuona nini hapa?

Hakuna tiba ya Mdondo  
inayofahamika. Njia pekee ni  
kuwakinga kuku ili wasipate ugonjwa.



Lakini ni jinsi gani tunaeweza kuwakinga kuku wasipatwe na  
ugonjwa? Jambo la muhimu ni kuwachanja dhidi ya ugonjwa wa  
mdondo.

Ni wakati gani tunapaswa kuwachanja kuku wetu? Kuku  
wachanjwe angalau mwezi mmoja kabla ya kipindi ambacho  
ugonjwa unategemewa kutokea.

Kuku gani wanaopaswa kuchanjwa? Ni muhimu kuchanja kuku  
ambao wana afya nzuri. Usihangaike kuchanja kuku mgonjwa,  
kwani chanjo haitamsaidia chochote maana utakuwa umechelewa.  
Chanjo haitibu kuku mgonjwa.

Chanjo haina madhara yoyote kwa kuku hata kwa  
binadamu. Baada ya kuchanjwa kuku anaweza akachinjwa na  
kuliwa bila kuleta madhara yoyote. Kuku aliyechanjwa huendelea  
kukua na kutaga mayai kama kawaida.

Chanjo ambayo tunaitumia kuwakinga kuku dhidi ya ugonjwa  
wa mdondo inaitwa I-2. Chanjo hii inatengenezwa hapa  
Tanzania mahususi kwa ajili ya kuku waliopo vijijini. Wakati  
mwingine inaweza kutunzwa nje ya jokofu kwa muda mfupi.  
Chanjo hii inafaa kwani hakuna majokofu ya kutosha vijijini.

# THIBITI UGONJWA WA MDONDO



**CHANJA KUKU WAKU DHIDI YA UGONJWA WA MDONDO  
KILA BAADA YA MIEZI 4  
KWA KUTUMIA CHANJO AINA YA 1-2**

Chanja Kuku		Hesabu Kuku Agiza chanjo	Chanjo inpatikana Karibu
<b>JANUARI</b>	<b>FEBRUARI</b>	<b>MARCH</b>	<b>APRILI</b>
J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28	J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30
<b>MEI</b>	<b>JUNE</b>	<b>JULAI</b>	<b>AGOSTI</b>
J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30	J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31
<b>SEPTEMBA</b>	<b>OKTOBA</b>	<b>NOVEMBA</b>	<b>DESEMBA</b>
J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30	J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30	J'pili J'tatu J'ne J'tano Aha Ijum J'mosi 1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31

## THIBITI UGONJWA WA MDONDO



CHANJA KUKU WAKU DHIDI YA UGONJWA WA MDONDO  
KILA BAADA YA MIEZI 4

KWA KUTUMIA CHANJO AINA YA I-2

Ghaqa Kuku	JANUARI	FEBRURI	Hesabu Naka Agas churjo	Ciriojo Inapitikana Kutoka
	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30
MIEJI	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31
JUNE	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31
SEPTEMBRA	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31
OKTOSBA	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31
NOVEMBRA	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31
DESEMBER	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31	1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 21 22 23 24 25 26 27 28 29 30 31

### Kielelezo 12.

#### Tone le jicho

Tuna nini hapa ?

Tunaona mtu ameshika kichwa cha kuku na anadondosha tone la chanjo katika jicho.

Njia bora ya kuchanja kuku dhidi ya mdondo ni kwa kuweka tone moja la chanjo katika jicho la kuku.


Ni ujuzi rahisi kwa wakulima kujifunza.

Kuku wa umri wote kuanzia kifaranga cha siku moja hadi kuku wenye umri mkubwa wapate tone moja katika jicho moja tu.


Angalia tena katika picha. Unaweza kuona nibu ya chupa ya chanjo inaelekezwa moja kwa moja katika jicho, hii ni muhimu ili kuhakikisha tone lenye ukubwa unaolingana limedondoshwa kwa kila kuku.

Kama inavyoonekana katika picha, ni rahisi kuchanja ikiwa mtu mmoja anakuwa amemshika kuku na mwagine anamchanja.

1



2




### **Kielelezo 13.**

### **Vipindi vya chanjo**

Nini kinaonyeshwa hapa?

Tuna kalenda yenyeye maelekezo.




Katika kalenda hii miezi ya Januari, Mei na Septemba imeandikwa kwa wino mweusi. Hii ni miezi ambayo chanjo inatakiwa kufanyika, hivyo basi kuku wanatakiwa kuchanjwa kila baada ya miezi minne.

Kwa kuchanja kuku kila baada ya miezi minne, kuku watakuwa na kinga dhidi ya mdondo mwaka mzima.

Vifaranga pia vitakuwa salama ikiwa chanjo itafanyika mara kwa mara.


Ili kuhakikisha kwamba tunayo chanjo ya kutosha wakati wa kuchanja ni vyema tuhesabu kuku tulionao na kuagiza dawa kabla ya kampeni ya chanjo.



## Kielelezo14.

### Kuhifadhi chanjo

Tunaweza kuona nini katika picha hii?



Tulisema hapo awali kuwa chanjo inaweza kukaa nje ya jokofu kwa muda, lakini ili kuhakikisha kuwa chanjo inafanya kazi vizuri inabidi tuitunze vyema.

Sehemu ya juu ya picha tunaweza kuona chanjo imeachwa juani.


Wakati chanjo hii ilipotumika kuwachanja kuku, hawakupata kinga na waliugua mdondo.


Ni muhimu kuweka chanjo sehemu kavu na yenyewe ubaridi. Isiwekwe sehemu yenyewe joto au mwanga wa juu. Ikiwezekana itunzwe kwenye jokofu.

Nyumbani kwako, unaweza kuweka chanjo katikati ikiwa imezungukwa na kata iliyobeba mtungi wa maji au ifunge kwenye kitambaa cha pamba, kilicholowanishwa na maji. Weka katika kivuli kama inavyoonyeshwa katika picha ya chini.

Pale ambapo unalazimika kusafirisha chanjo kwenda sehemu za mbali vijijini viringisha chanjo yako kenyе kitambaa kilicholowanishwa na maji na kuiweka ndani ya kikapu chenye kuingiza hewa na chenye mfuniko. Kamwe usiiweke kwenye mfuko wa plastiki au mfukoni.

Kumbuka kuchanja kuku wako kivulini.





### Kielelezo 15.

#### **Usiingize ndege mgeni wakati wa mlipuko**


Tunaweza kuona nini hapa?


Sasa tutazungumza ni jinsi gani tunaweza kuepuka kusambaza ugonjwa wa mdondo kutoka kijiji kimoja hadi kingine.

Mwanamke katika picha hii alinunua kuku sokoni na anamleta nyumbani kwake. Baada ya siku chache kuku wake wote wakafa.

Ni muhimu kuhakikisha kuwa huleti kuku wageni katika shamba lako wakati kuna mdondo katika vijiji vyaa jirani.

Hata kama hakuna ugonjwa wa mdondo maeneo ya karibu ni vizuri kuwatenga kuku wageni na wale wengine angalau kwa siku 10 ili kuhakikisha kuwa hawana ugonjwa ambao unaweza kasambaa kwa kuku wengine bandani.





### **Kielelezo 16.**

#### **Tenganisha kuku wanaoumwa kutoka walio na afya**

Nielezee unaona nini hapa?



Tunaona mwanamke ana kuku na mabanda mawili ya kuku.

Anafanya nini huyu mwanamke?

Anamwondoa kuku mgonjwa kutoka katika banda ili asiendelee kuambukiza ugonjwa kwa kuku wengine. Pindi kuku anapouagua, huwezi kumchanja. Unachoweza kufanya ni kumpa chakula, maji na sehemu nzuri ya kupumzikia.

Je wafugaji wengi wana mabanda mawili ya kuku?

Inawezekana hapana. Unawezaje kuwatenganisha kuku wagonjwa na wale ambao hawajaugua?



## Kielelezo 17.

**Haribu/tupa vitu vilivyoshambuliwa na vimelea vya ugonjwa kwa uangalifu**

Kitu gani kinatokea hapa?

Sehemu ya juu ya picha tunaona kuku waliokufa.

Utafanya nini mara kuku wengi watakapokufa kwa mdondo?

Ikiwa kuku atakuwa ni mgonjwa sana, ni vyema kumchinja.


Usisafirishe kuku wagonjwa au waliokufa kutoka katika nyumba moja kwenda nyingine au kwenda kwenye vijiji vipyta ambako kuku bado ni wazima.


Kuku yoyote aliye kufa kutokana na ugonjwa lazima achomwe moto au afukiwe.

Kama usipochoma au kufukia mzoga wote wa kuku hakikisha sehemu zisizotumika zinachomwa moto au kufukiwa. Sehemu hizo ni kama manyoya, mifupa au viungo vya ndani

Katika sehemu ya chini ya picha mwanamke anaweka manyoya na sehemu nyingine za kuku ndani ya shimo.

Kama kuku amekufa kutokana na mdondo. Usijaribu kuleta kuku wapya katika eneo hilo mpaka zipite angalau siku 30.






### **Kielelezo 18. Banda**

Unaweza kuona nini hapa?

Kuna aina mbili za mabanda ya kuku.

Una banda la kuku nyumbani kwako? Ni banda la aina gani?

Banda zuri la kuku litazuia kuku wasiliwe na ndege au wanyama wengine na pia litazuia kuenea kwa magonjwa kiurahisi kati ya kuku na kuku.



Kuku wakubwa wanaweza kuingia katika kibanda kilichonyanyuliwa juu. Sakafu katika banda hili imejengwa na miti ili kurahisisha kinyesi kupita kwenda chini.

Kuku wenye vifaranga hawawezi kulala kwenye mabanda yaliyanyuliwa labda kuwe kitu cha kufanya waweze kupanda. Vinginevyo lazima wawekwe kwenye nyumba iliyoko usawa wa ardhi. Ni muhimu kuhakikisha mlango wa banda ni mkubwa ili kuwezesha sakafu kufanyiwa usafi.

Hakikisha umetoa maganda kwenye miti ili kuzuia wadudu kama viroboto na chawa kujificha .

Safisha banda lako la kuku angalau mara moja kwa wiki. Baada ya kusafisha weka majivu katika sakafu na kuta kuzuia matatizo ya viroboto na chawa.

Ikiwa kama kumetokea mlipuko wa ugonjwa katika banda lako unashauriwa kulichoma lile banda la zamani na kujenga banda jipya na katika sehemu tofauti. Ikiwa hivyo haiwezekani basi usiruhusu kuku kuingia kwenye banda hilo angalau mpaka siku 30 zipite tangu siku ya mwisho ya ugonjwa ulipotoka.

Kielelezo 19. Lishe bora

Niambie unaona nini hapa?

Kwa kawaida kuku wa asili wanajitafutia chakula wenyewe.

Lakini kama tunaweza kuwapa chakula kidogo cha ziada, watazalisha zaidi.

Kuku anayekula vizuri atakuwa na uwezo wa kupambana na magonjwa na kupata kinga nzuri baada ya chanjo.

Lishe nzuri ni muhimu sana kwa vifaranga.

Tunavezaje kuwapa vifaranga chakula zaidi?

Tunaweza kuwapa mabaki ya chakula, chembe chembe za mchele au mahindi, majani mabichi, wadudu na maganda ya mayai na ya konokono yaliyosagwa. Pia wape maji safi.

Tenga katika picha hii linaweza kutumika kuwapa chakula vifaranga bila ya mtetea kukifikia. Hii ina maana kwamba kama huna chakula cha kutosha unaweza kuwalisha vifaranga chakula kidogo ulichokuwa nacho.





### **Kielelezo 20. Ikiwa kuna swali lolote muulize daktari wa mifugo au afisa ugani**

Nini kinatokea hapa?

Tuna wanawake wawili wanaongea na mmoja wao ana kuku mgonjwa.

Tunajua kwamba mdondo siyo ugonjwa pekee unaosababisha tu matatizo kwa kuku wetu.

Kama una maswali kila mara waulize madaktari au wataalamu wengine wa mifugo. Hawa wataalamu wako kwa ajili ya kukusaidia wewe.

Hapa ni mwisho wa mada yangu. Kama una maswali au maoni nitafurahi sana kuzungumza na wewe kuhusiana na hayo.

## **Shukurani**

Tunatoa shukurani zetu kwa ACIAR, AusAID, Wizara ya Maendaleo Ya Mifugo, Taasisi ya Utafiti wa Maradhi ya Mifugo, Idara ya Utafiti na mafunzo, Idara ya Huduma ya Mifugo, Vituo vya kanad vya ucchunguzi wa mifugo, Halmashauri za Wilaya za Dodoma vijijini, Dodoma mjini na Mtwara, Watumishi wa ofisi za mifugo za Wilaya ya Dodoma vijijini na mjini na Mtwara vijijini, Wafugaji wa kuku wa asili wa vijiji vya mkoa wa Dodoma na Mtwara.